

CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA



MWALIKO WA ZABUNI KWA AJILI YA KUPATA FUNDI WA KAZI YA KUJENGA DARASA LA WANAFUNZI MIA NNE (400) II NA NYUMBA YA WATUMISHI KATIKA CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019


Tarehe: 02 Julai, 2019

1. Mwaliko huu wa Zabuni unafuata Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Chuo cha Serikali Za Mitaa kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 uliochapishwa katika Gazeti la Manunuzi la Tanzania (Tanzania Procurement Journal - TPJ) toleo Na. ISSN: 1821 - 6021 Vol XI - No. 41 la tarehe 09 Oktoba, 2018.
2. Serikali ya Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Chuo cha Serikali za Mitaa katika mwaka wa fedha 2018/2019. Ikiwa inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo zitatumika kugharamia malipo halali chini ya mkataba ambao utatolewa katika mwaliko wa Zabuni hii.
3. Hivyo, Chuo cha Serikali za Mitaa kinakaribisha maombi kutoka kwa mafundi sanifu wa ujenzi ikiwa ni mtu binafsi au kikundi kinachotambulika na kusajiliwa kisheria kufanya kazi ya ujenzi, kazi hii inakusudiwa kufanyika kwa kutumia nguvu kazi (Force Account Procurement Method). Fundi sanifu anatakiwa kuwasilisha barua ya maombi ya kununua kitabu cha Zabuni kwa gharama ya **Shilingi Eelfu Hamsini (Tshs. 50,000.00)** tu kwa kila Zabuni kama ilivyofafanuliwa katika Jedwali hapo chini katika aya ya nne (4), ada hiyo italipwa moja kwa moja Chuo cha Serikali za Mitaa kupitia namba ya malipo **994490017117** ada hiyo haitarudishwa kwa fundi baada ya mchakato wa manunuzi (Non Refunderble fee).
4. Unakaribishwa kuleta zabuni yako ya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi (MMK) na kufafanuliwa ipasavyo katika sehemu ya II ya nyaraka hizi. Gharama ya kazi hii haitahusisha ununuzi wa vifaa vyoyote vya ujenzi badala yake changanua gharama ya ufundi tu kwa kazi zote ikizingatia michoro iliyoambatanishwa pamoja na zabuni hii.

Mchanganuo wa zabuni zinazo kusudiwa kutekelezwa katika mwaliko huu wa Zabuni ni kama ifuatavyo:-

Namba ya Zabuni.	Maelezo ya Kazi
ZABUNI NA. PA/080/2018/2019/W/04	Gharama ya ufundi wa kujenga darasa la kutumiwa wanafunzi 400 II
ZABUNI NA. PA/080/2018/2019/W/05	Gharama ya ufundi wa kujenga nyumba moja ya watumishi.

5. Waombaji watanunua vitabu vya zabuni na kupata maelezo ya zabuni husika katika Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kuanzia saa mbili kamili (2:00) asubuhi mpaka saa tisa kamili (9:00) jioni, kwa siku ya Jumatatu mpaka Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko hususani kwa kipindi cha zabuni hii tu.
6. Zabuni zote katika uhalisia wake (original) pamoja na nakala mbili (02) zinazofanana zilizojazwa zitawekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa " Namba na Jina la Zabuni. Pia ni lazima zipelekwe kwa;
Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo,
Jengo la Ofisi za Manunuzi (PMU) na Miliki (Estate),
S.L.P 1125,
DODOMA
7. Siku ya mwisho ya kuwasilisha na kupokea Zabuni ni Jumanne ya tarehe 09 Julai, 2019 kabla ya saa nane kamili (8:00) mchana. Zabuni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilishwa kwa zabuni husika mbele ya wawakilishi wa mafundi sanifu watakaoamua kuhudhuria katika ufunguzi wa zabuni ambao utafanyika katika Chuo cha Serikali za Mitaa, S.L.P 1125, **HOMBOLO - DODOMA** ndani ya ukumbi wa Maktaba kuu ya Chuo.
8. Kabla ya kujaza na kurudisha zabuni hii unashauriwa na kusesitizwa kuja kuona eneo ambapo ujenzi utafanyika ukisaidiwa na Mwenyekiti wa kamati ya Ujenzi kupitia Ofisi ya Afisa Miliki, hii ikiwa na lengo la kukusaidia Fundi kujaza zabuni hii kwa ukamilifu na usahihi unaokusudiwa.
9. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya zabuni, zabuni za kielektroniki, zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa zabuni, hazitakubaliwa kwa ajili ya kutathminiwa kwa hali yo yote ile.


Dkt. Mpamila Madale
MKUU WA CHUO

Mkuu wa Chuo
Page 2 of 2
Serikali za Mitaa-Hombolo
S. L. P. 1125,
DODOMA